

PHOTO: NARENDRA PATEL

BI RACHEL MWAJOHA

na
PETER KILEMBA

VIPINDI vya Television vina nia na lengo la kuelimisha mara nyingi ingawa vile vile vinatumbuiza. Vipawa vya wachezaji huwa kwa mara nyiingi ni vile walivyozaliwa navyo, kwani kuigiza tu pekee haitoshi. Bi Rachel Mwajoha bila ya shaka amezaliwa na kipawa hicho, ukamilifu katika wakati huu wamaisha yake. Alijiunga na vipindi vya Television Mombasa mwaka jana na ingaweja yeye ni mama watoto akiwa nyumbani kwake amekamilika kudhihirisha wajibu wa mama katika jamii yake, na hata kwa taifa lake. Wakati mwingi anachukua sehemu ya 'Mama' na shughuli hiyo huitekeleza kikamilifu bila dosari. Alisema ingawa watu wanafikiria kuwa michezo ta television kuwa kama 'sarakasi' tu lakini vile wanavyoonyesha wao ni MAFUNZO kwa jamii ambayo kwa mara nyingi hutoa mafunzo mema na kutimiza lengo lake kwa wananchi wote wa Kenya.

Utamaduni ushairi na shaha wa mashaha . . .

KAMA ilivyo makabila mbalimbali yana mila na desturi zao, Waswahili nao pia wanazo ambazo ni tafauti na zile za makabila mengine. Mila na desturi za Waswahili zinawapambanua na wengine kwa vile ni tafauti na hazifanani na za watu wengine.

Kila kabila - au taifa hutukuka an kujulikana kwa kuhifadhi na kubakisha mila na desturi zao, na ndiyo fahari yao na wao wenyewe ndio ambao wanazidumisha kwa kuzitilia nguvu zisalie milele na milele.

Shina la mila za Waswahili ni tungo (mashairi) zao ambazo ni chombo cha kueleza mambo yao. Mambo mengi ya mapisi (historia) yamekusanywa katika tungo.

T'ungo zinazotumiwa hivyo ni zinazotungwa kwa nidhamu, yaani zinafuata vina, mizani, vituo, vikomo na zimo katika bahari na mikondo tafauti tafauti. Maandishi yasiyokuwa na sifa hizi hayaitwi tungo. Tungo ni za aina ya mashairi, tendi (tenzi), nyimbo na kadhalika.

Lugha yenyewe ya Kiswahili aghlabu ina umbo la utungo, kwa mfano tukiangalia baadhi ya mithali ya Waswahili tutaona kuwa zina vina ambavyo vimezuka bila ya kudhamiriwa.

NA Ahmed Sheikh Nabhani

Angalia mpangilio wa mithali hii:-

- Mbio za sakafuni hushilia ukingoni
- Akili ni mali
- Mkaidi hafaidi ila siku ya Iddi

Na watoto wa Kiswahili wakiinukia watakuwa kwa lugha ya aina hii katika michezo yao ya kitoto. Pia nyimbo zao za kitoto zafuata vina na mizani kwa mfano-

- Mukipita mukiuyauya mwatakani twattaki majana ya nyuki mizingani

- Kobe, kobe la mt... teweo ni panya wa jana ...

Kwa hivyo mila hii ya... yaanza utotoni mpaka n... wa mtu mzima ambapo ... akawa mtungaji mzuri k... ya msingi huu alio nao ... udogoni. Zaidi yate... uhodari wa mtu na kud... mazuezi.

Kukifiliwa, kutia him... ushujaa wa kwenda ku... vita nakadhalika kunaf... kwa tungo. Pia kurai, ... haki, kuonyesha mape... machukivu lazima kun... wa kwa madhumuni ya ... butisha au kuhakikisha ... mambo yote hayo yan... dhika.

Basi utaona kuwa tu... muhimu kwa Waswahil... wale wasiokuwa na kipov... kutunga mashairi n.k. ... endea wale wajuwao w... we, kwa hatua baada ya ... mtu ajibidiishaye kuj... kitonga kutoka kwa wa... juwao siku moja atakua n... hodari.

Na ni hatua zipi atakaz... hata atambulike kuwa ni ... iri kamili? Hatua zenye... kua ataanza kupanda dar... kwanza na kuitwa fundizi ... akiendelea kuonyesha u... wake atakikia daraja ya ... na kuendelea mpaka atik... raja ya shaha, yaani mfalm... ushairi. Mwisho kabisa ik... kana aweza kuwa shah... mashaha, yaani mfalme w... falme wa ushairi.

Pindi kukiwa na arus... bayo kwa Waswahili ni sh... na kuchezwa ngoma ... mbali, ngoma ya gungu hu... wa, hapo huwepo mashin... kati ya mashaha ambao h... mika kujibizana kishairi ... kwa papo kwa njia ya ... fumbo. Kabla ya kuanza ... shindano watu hutoka ki... kwenda kumchukua shah... wakifika mlangoni pake h... imbia:-

- Shaha tumekuya kwa ... muamu msiu mpate na kut... dama siwate, twende tuka... gunguni.

Ingawa utungo huu ni w... sikazini yawezekana na p... ne wana tungu kama hiz... kisha kuchukuliwa na k... penye mashindano, yeye... mashaha wengine huanza ... shindano kwa mashairi ya ... fumbo na kujibizana. Ma... dano hayo yaweza kuend... mpaka asubuhi. Mashin... huwa ni chombo cha kupa... arusi na mangineyo.

RAIS M... APONGEZ... PWAN...

MWENYEKITI wa Ba... la Waisilamu nchini K... Haj Maalim Said bin ... amempongeza Mtuku... Daniel arap Moi kwa ... zwa kwake kama Ch... wa Chuo Kikuu cha ... na kumtakia kila la kh... ka juhudi zake zilizo... kuwapatia wananchi w... Kenya hakki sawa hat... Chuo Kikuu cha Nairob...

Akihutubia sherehe ... funguliwa kwa Chuo c... funzo mbali mbali huk... ni Maalim Said alisem... Kikuu cha Nairobi na ... vingine humu nchini vi... jibu mkubwa wa kute... kwa Taifa na watu wa K...

Coastweek *** JEMBE

SWAHILI CROSSWORD NO. 4

JEMBE
UNGA SAFI NO.1

WA MAHINDI

JINA.:..

SANDUKU LA POSTA...

....

KWENDA KULIA:	*KWENDA CHINI:*
2. Pasua,inua	1. Ashikwa na mshangao
7. Chimba kwa Kimombo	2. Aina ya mbegu fulani
8. Yakutizama wakati	3. Moja kati ya makontinenti ya dunia
9. Alioigiza	4. Na wao
12. Atenza nguvu	5. Kizazi cha ndege
14. Atia makali kisu	6. Baa
15. Aina ya viatu	10. Tunza mtoto
18. Dau zaidi ya moja	11. Ngoma kubwa
19. Kaghairi, kagoma	13. Onyesha, kataza
22. Sifa mbaya	
23. Sikukuu ya Kiislamu	
24. Ufupi wa ana shillingi tano	

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 2

KWENDA KULIA:
2. CHAMBA, 7. SAHAU, 9. OZA, 10. UHAI, 11. UFA, 12. FII, 13. ADUAA, 16. ILIKI, 19. CAT, 21. ANA, 22. CHOA, 23. AMU, 24. KAMAU, 25. UAMIRI.

KWENDA CHINI:
1. USUFII, 2. CHAI, 3. HAI, 4. AMA, 5. BOFU, 6. AZAA, 8. AHI, 11. UDI, 14. AMTAUA, 15. OKA, 17. LAMU, 18. INUA, 19. CHMI, 20. AOA, 22. CAR, 24. KI.

Washindi wa Fumbo La Kujaza Maneno No. 2:
(1) M. K. Khan wa Sanduku la posta 82035, Mombasa.
Washindi waombwa wafike Afisini mwa COASTWEEK.

Shindano la fumbo la kujaza maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi wawili wa kwanza kila mmoja atapatiwa bandali moja la Unga Wa Mahindi chapa Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LTD., pamoja na ATTA LTD., Mombasa.

Jawabu za fumbo hili, lipelekwe kwa muhariri COASTWEEK, sanduku la posta 87270, Mombasa, Kenya, siku ya Alhamisi tarehe 7.12.78 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.

KWA UFUPI

BARAZA la Mji wa Malindi litatumia zaidi ya shillingi 680,000 kwa upanuzi wa soko ya samaki katika sehemu hiyo. Alitamka Naibu wa Town Clerk wa sehemu hiyo, Bwana D. J. Randu. Shughuli za uvuvi Malindi ndio moja wapo wa shughuli muhimu za wenyeji wa sehemu hiyo. Alishukuru wizara ya serikali za wilaya kwa msaada huo.

MWENYEKITI wa Shirika la Meli nchini Kenya Bwana Mohammed Jahazi amesema kwamba Serikali ya Norway ikishirikiana na Chuo cha Mafunzo ya shughuli za Meli cha nchi hiyo itasaidia kuinua utumishi wa shughuli za meli

BARAZA la wilaya ya Taita Taveta limetoa mwito kwa serikali kurekebisha Hati ya sheria kuhusu Madini ili baraza hili liweze kupata kodi kutokana na shughuli za uchimbaji madini.

ROTARY Club ya Mombasa itajenga madarasa mapya katika shule ya Msingi ya St. Lwanga huko Changamwe kwa gharama ya shillingi 40,000/-. Alisema Mwenyekiti wa Umoja huo, Bwana Kishore Mehta.

SHIRIKA LA Viwanda na biashara nchini Kenya (ICDC) litatumia zaidi ya shillingi 12 millioni kwa upanuzi wa mipango ya maendeleo katika wilaya ya Taita Taveta.

AFISA Mkuu wa Idara ya Matibabu va Wanyama Pwani Dr. M. A. Fazal amesema kwamba idara yake itatumia aina bora ya Madawa ya kupambana na kupe wanaodhuru ng'ombe huko wilayani Taita Taveta. Alisema madawa hayo yataangamiza kabisa.

WAZAZI mjini Mombasa wameshauriwa kuwapeleka watoto wao katika shule za Nasary baada ya kufika umri wa miaka 3. Shauri hile limetolewa na Naibu wa Mkurugenzi wa idara ya huduma za jamii na nyumba ya Baraza la mji wa Mombasa, Bwana Ben Munyeki. Alisema Mombasa ina jumla ya Nasari skuli 13.

PHOTO: NARENDRA PATEL

BALOZI AFURAHIA MAENDELEO

UJASIRI na juhudi za watu wa Kenya katika ujenzi wa Taifa lao umepongezwa na Balozi wa Oman nchini Kenya Sheikh Salim Hakkim Al-Hassiby katika sherehe ya karamu ambayo alikuwa mgeni wa heshima.

Sheikh Hassiby alisema wananchi wa Kenya ni lazima kujivunia maendeleo yao ambayo ni mfano mkubwa katika Afrika. Alisema Elimu ndio msingi wa maendeleo na kutoa mwito kwa wazazi kuwaelimisha watoto wao kwani elimu ndio urithi bora zaidi.

Sherehe hiyo iliyoandaliwa na Umoja wa NUKEM ilihudhuriwa na Umati mkubwa huko Sakina. Hapo Balozi huyo anaonekana akihutubia waliofika. Wingine katika picha kutoka kushoto Sheikh Badi Muskat (Iman), Kadhi Mkuu (Kenya) Sheikh Abdalla Saleh Al-Farsy, na Mwenyekiti wa NUKEM Pwani, Sheikh Ali Amin.

KIUMBE NAKUUSIA

na
ABDUL SALIM HEMED,
Mvita

Mja tuza roho yako,
Utoe katika chako,
Kiasi uwezo wako,
kiumbe nakuusia,

Kutoa ni khairati,
Yenye kulinda hayati,
Shima yatoe manoti,
Kiumbe nakuusia,

Fakiri toa kalili,
Yatumie yako mali,
Haufai ubakhili,
Kiumbe Nakuusia,

Mali njia mojawapo,
Yategemea ambapo,
Mali yanakupa pepo,
Kiumbe nakuusia,

Jikaze sione dhiki,
Shetani simshiriki,
Mola atakubariki,
Kiumbe nakuusia,

Sighurike na dunia,
Mola alokujalia,
Si lazima kwa mamia,
Tengeza akhera yako.

Ambayo imetimia,
Akhera ukifikia,
Uwache kuyabania,
Tengeza akhera yako.

Na mwenyenacho zidia,
Kwa njia yake jalia,
Tahadhari nakwambia,
Tengeza akhera yako,

Ya uzuri na ubaya,
Utakavyo ya tumia,
Au moto wa hawiya,
Tengeza akhera yako.

Ushinde moyo sikia,
Toa chako saidia,
Na peponi kukutia,
Tengeza akhera yako.

Ukitumia vizuri,
Itakuepuka nari,
Tokeza kwa kila kheri,
Kiumbe nakuusia

Sidharau utajiri,
Ukitoa utapata,
Malipo utayakuta,
Kiumbe nakuusia

Yailahi yarazaki,
Rabi tupe riziki,
Tuitoe kila haki,
Kiumbe nakuusia

Twakuomba ...
Mola tutie imani,
Yailahi ya ...
Kiumbe nakuusia,

Amina Mola jalali,
Azimio letu hili,
Dua na iwe ...
Kiumbe nakuusia

Mali yako kwa sharia,
Na kila lenye udhia,
Utoe chako kwa nia,
Tengeza akhera yako.

Uzingatie wasia,
Ijapo kidogo pia,
Akhera yakungojea,
Tengeza akhera yako.

Mola yote yakwelea,
Isilamu sote pia,
Kwa moyo wa kuridhia,
Tengeza akhera yako.

Yetu kutukubalia,
Tuzidi kujitolea,
Yawe tulokusudia,
Tengeza akhera yako.

Wajao twahitajia,
Lizidi kuendelea,
Baraka kutuzidia,
Tengeza akhera yako.